Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (Kanuni za Udhibiti wa Matangazo ya Dawa za Binadamu na Mifugo)

TANGAZO LA SERIKALI Na. …………………… lililochapishwa tarehe …………………

SHERIA YA DAWA NA VIFAA TIBA

(SURA YA 219)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 95 na 122(l)(p))

KANUNI ZA UDHIBITI WA MATANGAZO YA DAWA ZA BINADAMU NA MIFUGO, 2025

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (Kanuni za Udhibiti wa Matangazo ya Dawa za Binadamu na Mifugo)

TANGAZO LA SERIKALI Na. …………………… lililochapishwa tarehe …………………

SHERIA YA DAWA NA VIFAA TIBA

(SURA YA 219)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 95 na 122(l)(p))

KANUNI ZA UDHIBITI WA MATANGAZO YA DAWA ZA BINADAMU NA MIFUGO, 2022

	MPANGILIO WA KANUNI
Kanuni	*Jina*
	SEHEMU YA KWANZA
	MASHARTI YA AWALI
1.	Jina
2.	Matumizi
3.	Tafsiri
	SEHEMU YA PILI
	UDHIBITI WA MATANGAZO
4.	Matangazo ya dawa
5.	Makatazo ya utangazaji wa dawa
6.	Maudhui ya nyenzo za matangazo
7.	Maombi ya kibali cha matangazo
8.	Kuhuisha kibali cha matangazo
9.	Mabadiliko kwenye nyenzo za matangazo
10.	Matangazo kwa wataalam wa afya
11.	Matangazo kulingana na makundi ya dawa
12.	Ulinganisho wa bidhaa
13.	Matangazo kwa umma
14.	Matangazo mafupi
15.	Usitishaji wa vibali
16.	Notisi ya kusitisha kibali cha matangazo
17.	Kusitisha au kufuta kibali bila notisi
18.	Kurejesha kibali
19.	Kukataa kutoa kibali

20.	Kubatilisha kibali
	SEHEMU YA TATU
	SAMPULI ZA KUFANYIA MATANGAZO
21.	Sampuli za bure
22.	Sampuli za dawa za tiba zenye madhara ya kulevya
23.	Zawadi, vishawishi na manufaa mengine
	SEHEMU YA NNE
	MATANGAZO KWENYE MITANDAO YA KIJAMII, TELEVISHENI NA VIPINDI VYA REDIO
24.	Matangazo kwa njia ya kimtandao
25.	Mitandao ya kijamii
26.	Vipindi vya Redio na Televisheni

	SEHEMU YA TANO
	MAONESHO, MAKONGAMANO NA MIKUTANO MINGINE
27.	Idhini ya kuendesha makongamano na mikutano mingine
28.	Makongamano ya kisayansi na mikutano mingine
29.	Wadhamini wa makongamano ya kisayansi au mikutano
	SEHEMU YA SITA
	UKAGUZI NA UDHIBITI
30.	Kaguzi zinazofanywa na Mamlaka
31.	Mamlaka ya Wakaguzi
	SEHEMU YA SABA
	UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU
32.	Kumbukumbu zitakazotunzwa na mwombaji
33.	Kumbukumbu zitakazotunzwa na Mamlaka
	SEHEMU YA NANE
	MASHARTI YA JUMLA
34.	Pingamizi la kusimamisha au kuondoa kibali
35.	Rufaa
36.	Adhabu
37.	Ufifilishaji makosa
38.	Kufutwa kwa Tangazo namba 160 la mwaka 2010

MAJEDWALI

	SEHEMU YA KWANZA MASHARTI YA AWALI
Jina	**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Udhibiti wa Matangazo ya Dawa za Binadamu na Mifugo, 2025 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
Matumizi	**2.** Kanuni hizi zitatumika kwenye udhibiti wa matangazo ya dawa za binadamu na mifugo pamoja na bidhaa za kibaiolojia, vipukusi na dawa za mitishamba zitakazotangazwa Tanzania Bara. Kanuni hizi hazitahusu dawa za asili.
Tafsiri	**3.** Katika kanuni hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo-
	"tangazo fupi" inamaanisha tangazo lililotengenezwa likionesha jina la kampuni, nembo au jina la bidhaa;
Sura 219	Sheria" inamaanisha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba;
	"tangazo" inamaanisha aina ya utangazaji, iwe katika uchapishaji, au kwa kuonesha notisi yoyote au kwa njia ya katalogi, orodha ya bei, barua, iwe waraka au iliyokusudiwa kwa kundi la watu au kwa maonesho ya picha au filamu ya sinema, au kwa njia ya sauti iliyorekodiwa, utangazaji wa sauti, au televisheni au njia nyingine yoyote ya mawasiliano ikiwemo mitandao ya kijamii, mawasiliano ya kielektroniki au kwa maneno yoyote yaliyotolewa hadharani;
	"Mamlaka" inamaanisha Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria, ambayo pia inajulikana kwa kifupi "TMDA";
	"vipukusi" maana yake ni bidhaa zenye kiambata hai kimoja au zaidi kilichoandaliwa kwa ajili ya kuharibu, kuzuia, kuondoa madhara au kukinga madhara au vinginevyo kuzuia madhara ya vimelea vya magonjwa kwa njia ya kemikali au biolojia. Kwa madhumuni ya kanuni hizi vipukusi vitajumuisha dawa za kuua vimelea kwenye ngozi na mazingira;
	"bidhaa za kibaiolojia" inamaanisha dawa zinazooteshwa na kusafishwa kutoka kwa midia kubwa za seli za bakteria au chachu, au mimea au seli za wanyama ikijumuisha chanjo, vichochezi vya ukuaji, vidhibiti kinga, kingamwili za monokloni, pamoja na bidhaa zinazotokana na damu;
	"tangazo linganishi"; maana yake ni tangazo linalolinganisha dawa mbili au zaidi kulingana na sifa za kiuchumi, utendaji, usalama au ubora;
	''kutoa dawa'' inamaanisha utoaji wa dawa kwa cheti au bila cheti kilichoandikwa na daktari wa binadamu, meno au mifugo;
	"umma" inamaanisha watu wengine zaidi ya wataalam wa afya;
	"dawa zinazotolewa bila masharti'' inaamanisha dawa yoyote ambayo matumizi yake hayahitaji maelekezo au maagizo kutoka kwa daktari

	wa binadamu, meno au mifugo;
	“wataalam wa afya” maana yake ni wanataaluma wa tiba ya binadamu, meno, wafamasia, maabara ya afya, wauguzi na mtu mwingine yeyote ambaye wakati wa kutekeleza majukumu yake ya kitaalam anaweza kuelekeza utolewaji au ugawaji wa dawa na kwa dawa za mifugo inahusisha madaktari na wataalam wengine wa mifugo;
	“dawa za mitishamba” inamaanisha mchanganyiko wowote uliowekewa lebo katika muundo wa dawa ulio na kemikali moja au zaidi kwenye kiasi kinachojulikana zitokanazo na viambata hai vya asili vitokanavyo na mimea bila kuhusisha dawa za asili;
	“mtengenezaji” inamaanisha ni mtu au kampuni inayojihusisha na uzalishaji,utayarishaji, usindikaji, uchanganyaji, uundaji, ujazaji, uboreshaji, ubadilishaji, ufungashaji na uwekaji lebo kwenye dawa;
	"madai ya kutibu" inajumuisha maelezo yoyote yanayohusu hali ya ugonjwa au sifa za bidhaa kuhusiana na matumizi yake ya matibabu;
	“dawa”, inamaanisha kitu chochote au mchanganyiko wa vitu vinavyotengenezwa, kuuzwa au kuwasilishwa kwa matumizi ya;
	(a) kutibu, kupunguza au kuzuia ugonjwa, maradhi, ulemavu wa mwili au akili, au dalili zake, kwa binadamu au mnyama;
	(b) kurejesha au kurekebisha afya ya akili kwa binadamu au mnyama;
	(c) kuua viini vinavyosababisha magonjwa katika maeneo ambayo dawa zinatengenezwa, kutayarishwa au kuhifadhiwa, hospitalini, vifaa na maeneo ya kufugia; au
	(d) kitu kingine chochote kinachotumika kama sehemu ya aya (a), (b) au (c); isipokuwa haijumuishi vifaa tiba, spea zake na vinavyoambatana;
	“matangazo ya dawa” yanamaanisha shughuli zozote za kutoa taarifa au kushawishi zinazofanywa na kampuni au kwa ridhaa yake kuhamasisha matumizi ya dawa yake;
	“dawa itolewayo kwa cheti cha daktari” inamaanisha dawa yoyote inayopaswa kutolewa kwa cheti cha dawa kilichotolewa na daktari wa binadamu, meno au mifugo au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa na mabaraza ya kitaaluma;
	“bidhaa” kwa madhumuni ya Kanuni hizi inamaanisha dawa za binadamu na mifugo, na vipukusi;
	“nyenzo za matangazo” inamaanisha kitu chochote kinachowakilisha sifa za bidhaa yoyote kwa namna yoyote kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya bidhaa;
	“tangazo la kukumbushia” inamaanisha tangazo lililotengenezwa kuwakumbusha wataalam wa afya na jamii kwa ujumla kuhusu uwepo wa bidhaa lakini haliwi na maelezo yoyote ya kuhamasisha matumizi ya bidhaa husika; na
	“dawa ya asili” inamaanisha mchanganyiko wowote wenye dawa inayotokana na ukaushaji, udondoaji, kusagwa, usindikaji, uendelezaji au ugandamizaji wa mimea asili au madini ya asili au sehemu yoyote ya mimea au madini hayo.

	SEHEMU YA PILI UDHIBITI WA MATANGAZO
Matangazo ya dawa	**4.** -(1) Shughuli yoyote inayofanyika kwa njia iliyoainishwa hapa chini itajumuisha utangazaji wa dawa; -
	(a) kutangaza;
	(b) shughuli za wawakilishi ikiwemo maelezo ya kuwasaidia na machapisho mengine yaliyochapishwa na kutumiwa na wawakilishi;
	(c) utoaji wa sampuli;
	(d) utoaji wa vishawishi ili kuandika cheti cha dawa kinachotolewa na daktari, utoaji dawa, kusambaza, kutumia, kupendekeza au kununua dawa kwa njia ya zawadi, kutoa dawa kwa ahadi ya kunufaika au motisha kwa njia ya fedha au zawadi;
	(e) utoaji wa ukarimu kwa madhumuni ya kutangaza;
	(f) udhamini wa mikutano ya matangazo;
	(g) kudhamini mikutano ya kisayansi ikiwa ni pamoja na kulipia safari na malazi;
	(h) kutoa taarifa kwa jamii moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja;
	(i) matangazo mengine yote ya mauzo kwa namna yoyote ile, kama vile kushiriki katika maonesho, matumizi ya kaseti za sauti, filamu, rekodi, redio, televisheni, mawasiliano kwa njia ya mtandao na kielektroniki au njia nyingine yoyote ya mawasiliano.
	(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), shughuli zifuatazo hazitakuwa matangazo ya dawa;
	(a) majibu ya maswali binafsi yanayotolewa kwa watoa huduma wa afya au watumishi kwa kujibu mawasiliano maalum kutoka kwao kama ya uchunguzi au maoni;
	(b) taarifa ya kweli na sahihi, nyenzo rejea kuhusu dawa zilizoidhinishwa kuhusiana na kuonesha mabadiliko ya kifungashio, maonyo ya athari mbaya za dawa, katalogi za biashara na orodha za bei, ili mradi hazijumuishi maelezo ya tiba ya bidhaa;
	(c) muhtasari wa sifa za bidhaa;
	(d) uwekaji wa lebo kwenye dawa na vipeperushi vilivyoambatishwa ili mradi taarifa husika hazitangazi dawa; na
	(e) taarifa zinazohusiana na afya ya binadamu au magonjwa ili mradi hakuna rejea, ama moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, kwa bidhaa husika.
Makatazo ya utangazaji wa dawa	**5.** -(1) Bidhaa yoyote haitatangazwa kama haijasajiliwa na Mamlaka.
	(2) Vifungashio na lebo vitakuwa na taarifa inayoendana na ile iliyoidhinishwa wakati wa usajili wa bidhaa.

	(3) Bidhaa haitatangazwa kwa namna inayopotosha au inayolenga kupotosha moja kwa moja au kwa hisia kuhusu sifa, kiasi, mchanganyiko, usalama au ufanisi kwa kadiri itakavyokuwa.
	(4) Matangazo ya bidhaa kwa umma yasiwe na picha za viungo vya ndani au vya uzazi.
	(5) Lugha inayoleta au inayoweza kupotosha au kudanganya au kuleta hofu kwa mtu binafsi au jamii hairuhusiwi.
	(6) Tangazo lolote linaloshawishi au kuvutia watoto kutumia bidhaa yoyote haliruhusiwi.
	(7) Tangazo la umma kwa ujumla halitarejea Sheria, Mamlaka, mtumishi yeyote wa Mamlaka, nembo au alama ya Serikali.
	(8) Utangazaji wa dawa kwenye masoko na vyombo vya usafiri wa umma hauruhusiwi chini ya Kanuni hizi.
Maudhui ya nyenzo za matangazo	**6.** -(1) Maudhui ya nyenzo za matangazo yasiwe yenye upendeleo, yawe sahihi, yenye taarifa ya kueleweka, yenye taarifa za karibuni, yenye kukubalika na yalingane na taarifa iliyoidhinishwa wakati wa usajili wa bidhaa.
	(2) Nyenzo za matangazo zisiwe na taarifa za kupotosha au zisizoweza kuthibitishwa au zilizofichwa kuhusu ubora, usalama, na ufanisi au thamani inayoweza kushawishi matumizi ya bidhaa yasiyofaa kiafya au yanayoweza kusababisha hatari.
	(3) Nyenzo za matangazo ziwe kwa lugha ya Kiingereza, Kiswahili au zote kwa pamoja.
Maombi ya kibali cha matangazo	**7.** -(1) Ombi la kibali cha idhini ya kutumia nyenzo za matangazo kwa Mamlaka liwasilishwe na viambatisho vifuatavyo:- (a) fomu ya maombi iliyojazwa kikamilifu kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali la kwanza** la Kanuni hizo; (b) nakala ya tangazo litakalotumika; na (c) ada ya maombi ya kibali iliyoainishwa katika Kanuni za Ada na Tozo zinazotumika.
	(2) Kulingana na kanuni ndogo ya (1) (c), ada ya ombi la kibali itatozwa kwa kila nyenzo ya matangazo.
	(3) Mamlaka itafanya tathmini ya ombi la kibali cha kutangaza dawa kulingana na miongozo iliyopo.
	(4) Mamlaka ikiridhika kwamba tangazo linalopendekezwa linakidhi matakwa yaliyoainishwa katika Kanuni hizi, itatoa kibali cha matangazo kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Pili** la Kanuni hizi.
	(5) Kulingana na kanuni ndogo ya (4), kibali cha matangazo ya dawa kitakua hai kwa kipindi cha miaka miwili.
Kuhuisha kibali cha matangazo	**8.** -(1) Ombi la kuhuisha kibali cha matangazo liwasilishwe ndani ya siku thelathini kabla ya ukomo wa matumizi ya kibali hicho kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni ya 7 (4).
	(2) Kulingana na kifungu kidogo cha (1), ombi la kuhuisha kibali cha matangazo liambatishwe na: - (a) fomu ya maombi ya kuhuisha iliyojazwa kikamilifu kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali la Kwanza** la Kanuni hizi;

	(b) nakala ya tangazo litakalotumika; na (c) ada ya maombi ya kibali kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Ada na Tozo zinazotumika.
Mabadiliko kwenye nyenzo za matangazo	**9.** - (1) Mabadiliko yoyote kwenye tangazo lililoidhinishwa yatatolewa taarifa kwa Mamlaka na kutekelezwa kwa idhini ya Mamlaka.
	(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), mabadiliko yoyote yatakayohusisha kuongeza au kubadili ujumbe kwenye tangazo yatachukuliwa kama tangazo jipya na hivyo yatahitaji kuombewa kibali upya.
Matangazo kwa wataalam wa afya	**10.** Tangazo kwa wataalam wa afya litakuwa na taarifa ambazo zinapaswa kuendana na muhtasari wa sifa za bidhaa ulioidhinishwa ikiwa ni pamoja na:
	(a) jina la kibiashara;
	(b) jina la kiambata hai kwa kutumia majina ya kimataifa yasiyo na umiliki au jina la jenesi la dawa;
	(c) kiasi cha kiambata hai katika muundo na utaratibu wa utoaji dozi;
	(d) jina la viambata vingine vinavyojulikana kusababisha madhara;
	(e) matumizi ya dawa yaliyoidhinishwa;
	(f) muundo na utaratibu wa utoaji dozi;
	(g) athari na madhara makubwa yatokanayo na matumizi ya dawa;
	(h) tahadhari, zuio la utumiaji wa dawa na maonyo;
	(i) mwingiliano mkubwa wa dawa;
	(j) jina na anuani ya mtengenezaji; na
	(k) marejeo ya taarifa za machapisho ya kisayansi inapobidi.
Matangazo kulingana na makundi ya dawa	**11.** -(1) Dawa za tiba zenye madhara ya kulevya, dawa zinazotolewa kwa cheti cha daktari na dawa pekee za kwenye famasi kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za makundi ya dawa hazitatangazwa kwa umma.
	(2) Bila kuathiri masharti ya Kanuni ndogo ya (1), dawa itolewayo kwa cheti cha daktari inaweza kutangazwa kwa wataalam wa afya.
	(3) Dawa zinazouzwa bila masharti zinaweza kutangazwa kwa wataalam wa afya na umma.
	(4) Mamlaka inaweza kuidhinisha dawa zitolewazo kwa cheti cha daktari kutangazwa kwa manufaa ya umma.
Ulinganisho wa bidhaa	**12.** -(1) Ulinganisho wa bidhaa kwa madhumuni ya mashindano hauruhusiwi.
	(2) Ulinganisho wa bidhaa unaweza kuruhusiwa endapo hautakuwa wa kudhalilisha, utakuwa kweli, wa haki, wenye ushahidi na usiopotosha, kwa msisitizo au njia nyingine yoyote.
	(3) "Kulinganisha bila ushahidi" kudai kuwa bidhaa ni bora,

	yenye nguvu, au na inayoandikwa kwa wingi na madaktari hairuhusiwi.
Matangazo kwa umma	**13.** -(1) Matangazo yanayotolewa kwa umma yanaweza kuwa na-
	(a) jina la jenesi na jina la biashara;
	(b) jina la kiambata hai kwa kutumia majina ya kimataifa yasiyo na umiliki;
	(c) matumizi ya dawa yaliyoidhinishwa;
	(d) tahadhari, zuio la utumiaji wa dawa na maonyo;
	(e) jina na anuani ya mtengenezaji;
	(f) utaratibu wa utoaji dozi;
	(g) maneno “maumivu yakizidi muone daktari”;
	(2) Matangazo kwa umma yatazingatia yafuatayo;
	(a) kuwasaidia watu kufanya maamuzi wakiwa na taarifa sahihi kuhusu uchaguzi na matumizi ya dawa inayotumika kihalali bila kutumia cheti cha dawa kutoka kwa daktari;
	(b) mahitaji halali ya watu kupata taarifa kuhusu afya zao; na
	(c) kutotumia mahitaji ya watu ya kiafya kujinufaisha.
Matangazo ya kukumbushia	**14.** Matangazo ya kukumbushia yaainishe angalau jina la jenesi, jina la kibiashara, jina la kimataifa lisilo na umiliki au jina la kila kiambata hai, na jina na anuani ya mtengenezaji bila kuwa na madai ya kushawishi matumizi ya dawa.
Usitishaji wa vibali	**15.** Mamlaka inaweza kusitisha kibali cha matangazo ya dawa iwapo itajiridhisha kuwa-
	(a) dawa iliyosajiliwa imetangazwa katika namna ambayo ni ya uongo au ya kupotosha au haikidhi masharti ya Sheria na Kanuni hizi;
	(b) mwenye kibali amekiuka Kanuni hizi au masharti mengine kwenye Sheria;
	(c) mwenye kibali alitoa maelezo ya uongo au ya kupotosha au kutatanisha wakati wa kuomba kibali; au
	(d) kibali hakikuhuishwa ndani ya muda uliowekwa.
Notisi ya kusitisha kibali	**16.** -(1) Kusitisha kibali kutafanyika kwa kutoa notisi ya maandishi.
	(2) Notisi ya kusitisha kibali kama ilvyoainishwa kwenye **jedwali la tano** la kanuni hizi-
	(a) itaeleza sababu ya kusitisha kibali, mapendekezo ya hatua za kuchukua na muda wa kukamilisha hatua hizo; na
	(b) itamtaka mwenye kibali kutoa utetezi dhidi ya kusudio la usitishwaji.
Kusitisha au kufuta kibali bila notisi	**17.** -(1) Mamlaka inaweza kufuta au kusitisha kibali bila notisi iwapo itaonekana inafaa kufanya hivyo ili kulinda afya ya jamii.
	(2) Iwapo kibali kitasitishwa au kufutwa, mwenye kibali anaweza kuomba kwa maandishi, kibali kirejeshwe.

	(3) Mamlaka inaweza, ndani ya siku (30) kutoka siku ya kupokea ombi la kurejeshewa kibali kilichofutwa au kusitishwa, kupitia upya maamuzi yake.
Kurejesha kibali	**18.** Kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya 15 na 17, Mamlaka, baada ya kujiridhisha kwamba sababu zilizopelekea kusitisha au kufuta kibali zimerekebishwa au sababu hizo hazikua na mashiko, inaweza kurejesha kibali hicho.
Kutokutolewa kwa kibali	**19.** -(1) Mamlaka inaweza isitoe kibali kama ikijiridhisha kwamba-
	(a) imepitia maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kanuni ya (7) na kubaini kuwa mwombaji hajakidhi masharti ya Kanuni hizi; na
	(b) nyenzo za matangazo husika hazikidhi sera, masharti, kanuni na sheria nyingine za nchi.
	(2) Kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (1), pale ambapo Mamlaka haitatoa kibali cha matangazo, Mkurugenzi Mkuu atamtaarifu mwombaji kwa maandishi juu ya uamuzi na sababu za uamuzi huo.
	(3) Kutokutolewa kwa kibali kutazuia matangazo ya dawa husika nchini.
	(4) Taarifa na sababu za kukataliwa kibali zinaweza kutolewa kwa umma.
Kubatilisha kibali	**20.** -(1) Mamlaka inaweza kufuta au kubatilisha kibali cha matangazo iwapo-
	(a) matangazo yatakayotangazwa yatakua si kwa manufaa ya umma;
	(b) bidhaa za dawa husika zimepigwa marufuku Tanzania bara;
	(c) uhalali wa usajili wa dawa husika umefikia ukomo; au
	(d) usajili wa dawa husika umesitishwa kwa zaidi ya miezi sita.
	(2) Kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (1), notisi ya kufuta kibali itatolewa kwa mwenye kibali kwa maandishi kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali la Tano** la Kanuni.

	SEHEMU YA TATU SAMPULI KWA AJILI YA MATANGAZO
Sampuli za bure	**21.** -(1) Mtu hataruhusiwa kuuza au kusambaza sampuli za bure za dawa kwa umma kwa madhumuni ya kuzitangaza.
	(2) Sampuli za bure za dawa zitatolewa tu kwa daktari wa binadamu, meno, mifugo au mfamasia kwa zile ambazo wanaruhusiwa kuandika au kutoa.
	(3) Sampuli za bidhaa zitapaswa kuwa na lebo inayoonekana kwa uwazi au ziwekewe alama "Sampuli za Bure-Haziuzwi" na lazima ziambatishwe na nakala ya maelezo ya sifa za bidhaa iliyoidhinishwa.
	(4) Sampuli za bure za bidhaa lazima ziwe katika kifungashio kidogo zaidi kilichosajiliwa na Mamlaka.

Sampuli za dawa za tiba zenye madhara ya kulevya	**22.** Sampuli za dawa za tiba zenye madhara ya kulevya hazitatolewa kwa wataalam wa afya na kwa umma.
Zawadi na vishawishi	**23.** -(1) Mtu hataruhusiwa kutoa zawadi, manufaa au faida ya kifedha kwa wataalam wa afya, familia zao kama kichocheo cha kuandika cheti cha dawa, kusambaza, kusimamia, kupendekeza au kununua bidhaa yoyote.
	(2) Zawadi au tuzo haitatolewa kwa wataalam wa afya katika namna inayosaidia kuitangaza bidhaa isipokuwa kama zawadi hiyo ni ya gharama ndogo na inafaa kwa matumizi ya kitaalam au kazi zao.
	SEHEMU YA NNE
	MATANGAZO KWENYE MITANDAO YA KIJAMII, TELEVISHENI NA VIPINDI VYA REDIO
Matangazo ya dawa kwenye mtandao	**24.** -(1) Wachapishaji wa tovuti wahakikishe matangazo yote yanayochapishwa kwenye mtandao hayakiuki Kanuni hizi.
	(2) Matangazo ya dawa zinazotolewa na cheti cha daktari kwa umma kupitia mitandao na njia nyingine za kidigitali hayataruhisiwa chini ya Kanuni hizi.
Mitandao ya kijamii	**25.** -(1) Chini ya Kanuni hizi, mitandao ya kijamii itajumuisha Facebook, YouTube, Twitter, WhatsApp, Instagram, Telegram, LinkedIn, Snapchat, Reddit, Blogs, TikTok, televisheni za mtandaoni au njia nyingine yoyote.
	(2) Matangazo ya dawa za tiba zenye madhara ya kulevya, dawa zinazotolewa kwa cheti cha daktari na dawa pekee za famasi kwenye mitandao ya kijamii iliyorejewa kwenye kanuni ndogo ya (1) hayataruhusiwa.
	(3) Matangazo ya dawa zinazouzwa bila masharti kwenye mitandao ya kijamii iliyorejewa kwenye kanuni ndogo ya (1) inaweza kuruhusiwa baada ya kuidhinishwa na Mamlaka.
Televisheni na vipindi vya redio	**26.** -(1) Mtu hataruhusiwa kutangaza dawa kwenye televisheni au kipindi cha redio bila kibali cha maandishi kutoka Mamlaka.
	(2) Kutokana na kanuni ndogo ya (1), maombi ya idhini ya kutangaza dawa yawasilishwe kwa mujibu wa kanuni ya saba (7) katika Kanuni hizi.
	SEHEMU YA TANO
	MAONESHO YA BIASHARA, MAKONGAMANO NA MIKUTANO MINGINE
Kibali cha maonesho ya biashara	**27.** -(1) Maombi ya vibali vya maonesho ya biashara yatawasilishwa na mwombaji kwa kuambatisha- (a) fomu iliyojazawa kikamilifu kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Tatu** la kanuni hizi; na (b) ada ya maombi kwa waombaji wa nje ya nchi kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Ada na Tozo zinazotumika.

	(2) Baada ya kupitia maombi ya matangazo, Mamlaka inaweza kutoa kibali kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Nne** la Kanuni hizi.
	(3) Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), ombi la maonesho ya biashara litapaswa kuwasilishwa ndani ya siku 14 kabla ya maonesho kuanza.
	(4) Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2), dawa zinazoweza kuuzwa bila masharti ya cheti cha daktari zinaweza kuruhusiwa kuuzwa kwa umma wakati wa maonesho.
	(5) Pale ambapo ombi linalorejewa kwenye kanuni ndogo ya (1) limeombwa na kundi la makampuni, kila kampuni itapaswa kulipia ada ya maombi hayo.
	(6) Dawa zinazouzwa bila masharti ya cheti cha daktari zilizorejewa kwenye kanuni ndogo ya (4) zitalipiwa ada ya uingizaji nchini wa dawa kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Ada na Tozo zinazotumika.
	(7) Mamlaka inaweza kutoa kibali maalum cha maonesho kwa mwombaji yeyote anayetaka kuonesha dawa ambazo hazijasajiliwa.
	(8) Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (7), sampuli zisizozidi tano kwa kila dawa katika kifungashio cha kibiashara zinaweza kuruhusiwa kuoneshwa isipokuwa zitatakiwa ziwekwe alama “Haziuzwi”.
Makongamano na mikutano mingine	**28.** -(1) Mtu hataruhusiwa kupanga au kufanya makongamano au mkutano bila kibali kilichotolewa na Mamlaka kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali la Nne**.
	(2) Mtu anayetaka kufanya makongamano au mikutano kama hiyo anatakiwa kuwasilisha ombi kama lilivyoainishwa kwenye **Jedwali la Tatu** la Kanuni hizi.
	(3) Uwasilishaji wa mada katika makongamano lazima uwe wenye ukweli, sahihi, bila kuficha na usiopendelea upande wa bidhaa ya kampuni yoyote.
	(4) Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2), uuzaji wa bidhaa yoyote kwenye makongamano au mikutano hiyo hautoruhusiwa.
Wadhamini wa maonesho ya kisayansi au mikutano mingine	**29.** Udhamini wa makongamano ya kisayansi au mikutano mingine au uwezeshaji wa wataalam wa afya kushiriki katika makongamano au mikutano mingine haupaswi kuambatana na masharti ya kutangaza dawa.
	SEHEMU YA SITA
	UKAGUZI NA UDHIBITI
Ukaguzi	**30.** -(1) Mamlaka inaweza kufanya ukaguzi wa nyenzo za matangazo wakati wowote katika majengo ya biashara, mipaka ya forodha, maonesho na viwanja vya maonesho, mitandao ya kijamii, mabango ya nje, vituo vya afya au katika jengo lolote pindi itakapohitajika.
	(2) Mamlaka inaweza kutoa notisi kwa mmiliki wa nyenzo za matangazo kumtaka atoe taarifa inayohusu uzingatiaji wa matakwa ya Kanuni hizi ndani ya muda utakaobainishwa kwenye notisi hiyo.

	(3) Ukaguzi wowote utakaofanywa na Mamlaka kwa mujibu wa Kanuni hizi katika Tanzania bara utachukuliwa kama ni ukaguzi wa nyenzo za matangazo katika maeneo ambayo shughuli za matangazo zinafanyika.
	(4) Mamlaka inaweza kuteua wakaguzi kwa mujibu wa sheria ili kutekeleza kazi zilizoainishwa katika Kanuni hizi na kuainisha vigezo vya masharti ya uteuzi kwa kadiri inavyoona inafaa.
Mamlaka ya wakaguzi	**31.** Ili kuhakikisha kwamba Kanuni hizi zinazingatiwa na ukaguzi unafanyika, mamlaka ya wakaguzi yatakuwa kama yalivyoainishwa kwenye Sheria.
	SEHEMU YA SABA
	UTUNZAJI KUMBUKUMBU
Kumbukumbu zitakazotunzwa na mmiliki	**32.** -(1) Mwombaji atakua na wajibu wa kutunza sampuli za matangazo, kutoa taarifa za matangazo kwa Mamlaka na kutekeleza uamuzi wowote utakaoelekezwa kuhusu matangazo ya dawa.
	(2) Mamlaka itakua na uwezo wa kuomba nakala ya tangazo lolote lililochapishwa kutoka kwa mtu yeyote aliyehusika na uchapishaji huo.
	(3) Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2), watangazaji wote watahakikisha nakala za matangazo yote zinatunzwa kwa niaba yao au na wao wenyewe.
	(4) Kumbukumbu zinazorejewa katika Kanuni hizi zitatunzwa kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu tangu kuisha kwa uhalali wa kibali.
Kumbukumbu zitakazotunzwa na Mamlaka	**33.** Mamlaka itatunza taarifa zote za kumbukumbu inazopokea zinazohusiana na nyenzo na matangazo ya dawa hasa zinazohusiana na- (a) idhini zote zitakazotolewa chini ya Kanuni hizi; (b) amri ya kutekeleza masharti ya mambo yote yanayohusiana na matangazo ya dawa; (c) ukaguzi au maombi ya taarifa zinazohusiana na matangazo ya dawa; na (d) taarifa nyingine zozote kama Mamlaka itakavyoona inafaa.
	SEHEMU YA NANE
	MASHARTI YA JUMLA
Pingamizi la kusitisha au kufuta kibali	**34.** -(1) Mwenye kibali ambaye-
	(a) Anapinga kusimamishwa au kufutwa kwa kibali au taarifa yoyote iliyotolewa; au
	(b) Anapinga kukataliwa kwa kibali au kuwekwa kwa sharti lolote, anaweza kumjulisha Mkurugenzi Mkuu kuhusu nia yake hiyo kwa maandishi au kwa kufika mbele na kusikilizwa na mtu aliyeteuliwa na Mkurugenzi Mkuu kwa madhumuni hayo.

	(2) Taarifa ya pingamizi kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) iwasilishwe ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya uamuzi ulipotolewa, Mamlaka inaweza kuongeza muda wa kuwasilisha pingamizi usiozidi siku saba baada ya kuombwa na kupewa sababu za kutosha.
	(3) Pale ambapo Mamlaka itapokea taarifa ya pingamizi kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), itateua mtu wa kushughulikia pingamizi hilo.
	(4) Mtu aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3) atapanga utaratibu utakaofuatwa kwa kuzingatia uzito wa pingamizi lolote.
	(5) Mtu aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3) atapaswa kuzingatia maelezo ya pingamizi yaliyoandikwa au ya mdomo yaliyotolewa na mmiliki wa kibali katika kushughulikia pingamizi lake, na atatoa mapendekezo kwa Mamlaka.
	(6) Mapendekezo yatakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni ndogo ya (5) yatawasilishwa kwa maandishi kwa Mamlaka, na nakala itatolewa kwa mmiliki wa kibali au mwakilishi wake aliyemteua.
	(7) Mamlaka itazingatia mapendekezo yoyote yaliyofanyika kwa mujibu wa Kanuni ndogo ya (5).
	(8) Mkurugenzi Mkuu atamjulisha ndani ya siku kumi na nne mmiliki wa kibali endapo anakubali mapendekezo yaliyotolewa kwa kufuata kanuni ndogo ya (5); pale ambapo hakubaliani atatoa sababu za uamuzi huo.
	(9) Pale Mkurugenzi Mkuu atakapojulishwa kuhusu pingamizi kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) (a) kabla ya tarehe ya ukomo wa notisi kuanza kutumika, notisi ya pingamizi haitatekelezwa hadi;
	(a) Mtu aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3) atapaswa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi na kutoa mapendekezo: na
	(b) Mkurugenzi Mkuu amemjulisha mmiliki wa kibali kuhusu uamuzi wake kulingana na mapendekezo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (8).
	(10)Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (9), pale Mkurugenzi Mkuu atakapojulishwa kuhusu pingamizi kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1)(a) ndani ya muda ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (2) kuhusu kusimamishwa, kubatilishwa au notisi nyingine ambayo tayari imeshaanza kutumika tarehe ambayo taarifa hiyo ilitolewa kusimamishwa, kubatilishwa au notisi ambayo pingamizi limefanywa itakoma kutumika hadi:
	(a) Mtu aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3) atapaswa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi na kutoa mapendekezo: na
	(b) Mkurugenzi Mkuu amemjulisha mmiliki wa kibali kuhusu uamuzi wake kulingana na mapendekezo kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (8)
	(11) Masharti ya kanuni ndogo ya (10) hayatatumika ikiwa:
	(a) notisi ya kusimamishwa, kufutwa notisi au notisi nyingine iliyotolewa imeanza kutekelezwa kwa mujibu wa Kanuni hizi; na

	(b) kwa hali yoyote ile pale Mkurugenzi Mkuu ataona kwamba ni muhimu kwa maslahi ya umma kusimamisha, kufuta au notisi nyingine kuanza kutumika katika tarehe iliyotajwa awali atatoa taarifa ya maandishi kwa wamiliki wa vibali husika.

Rufaa	**35.** -(1) Mtu yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi wa Mamlaka anaweza, ndani ya siku sitini tangu kupata nakala ya uamuzi, kukata rufaa ya maandishi kwa Waziri.
	(2) Mrufani atatoa nakala ya rufaa kwa Mamlaka ambapo ndani ya siku kumi na nne Mamlaka itawasilisha majibu ya kimaandishi kwa Waziri na nakala kwa Mrufani.
	(3) Pale Waziri atakaporidhika kwamba kuna hoja ya kujibu anaweza kuita wahusika kuleta nyaraka za ziada au kufanya uamuzi wa kukubali au kufuta rufaa.
Makosa na adhabu	**36.** Mtu yeyote anayekiuka au anayeshindwa kufuata Kanuni hizi moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja kumsaidia mtu mwingine kufanya kosa chini ya Kanuni hizi atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atapewa adhabu iliyowekwa kwa mujibu wa Sheria.
Kufifilisha makosa	**37.** -(1) Mkurugenzi Mkuu, Mkaguzi au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa anaweza, kwa kufuata na kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi, ikiwa ataridhika kwamba mtu ametenda kosa chini ya Kanuni hizi, atafifilisha kosa hilo kwa kupokea kutoka kwa mkosaji kiasi cha fedha ambacho kosa limetendwa.
	(2) Kiasi cha fedha kitakacholipwa chini ya kanuni ndogo ya (1) kitakuwa ni theluthi mbili ya kiwango cha juu cha faini kwa kosa hilo ilivyoainishwa katika Sheria.
	(3) Mamlaka ya kisheria kwa mujibu wa Kanuni hizi yatatumika pale ambapo mtuhumiwa atakiri kwamba ametenda kosa na atakubali kwa maandishi kwa kujaza fomu ya kufifilisha makosa iliyoainishwa kwenye **Jedwali la Sita** la Kanuni hizi.
	(4) Mkurugenzi Mkuu au mkaguzi aliyepewa mamlaka ya kisheria chini ya Kanuni hii atampa risiti baada ya kupokea malipo kutoka kwa mtu anayelipa kiasi cha fedha chini ya kanuni ndogo ya (2).
	(5) Kiasi cha fedha chini ya Kanuni hii kitalipwa kwa Mamlaka.
	(6) Mtu yeyote akishtakiwa mahakamani kwa kosa lolote chini ya Kanuni hizi, itakuwa ni utetezi endapo mtu huyo atathibitisha kuwa kosa analoshitakiwa nalo lilififilishwa chini ya Kanuni hii.
Kufutwa kwa TN. 160	**38.** Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi (Udhibiti wa matangazo ya dawa na mitishamba) Kanuni, 2010 zimefutwa

la mwaka 2010	

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 7 (1) na 8(2))

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

FOMU YA MAOMBI YA KUIDHINISHA NYENZO ZA MATANGAZO

ZINGATIA: Ni kosa kutoa taarifa ya kupotosha au tamko la uongo.

(Taarifa zote zinazotolewa katika fomu hii na mwombaji zinapaswa zichapwe au ziandikwe kwa herufi kubwa)

Taarifa za mwombaji

Jina la mwombaji:	
Anuani:	
Postikodi:	
Nambari ya simu ya mezani:	
Nambari ya simu ya mkononi:	
Barua pepe:	
Akaunti ya mtandao wa kijamii (*kama inahusika*)	

Taarifa za mdhamini (kama ni tofauti na za mwombaji)

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (Kanuni za Udhibiti wa Matangazo ya Dawa za Binadamu na Mifugo)

Jina la mdhamini:	
Anuani:	
Postikodi:	
Nambari ya simu ya mezani:	
Nambari ya simu ya mkononi:	
Barua pepe:	

Taarifa za dawa

Kundi la dawa	Weka alama ya vema pale inapofaa
Dawa itolewayo kwa cheti cha daktari	( )
Dawa Pekee ya Famasi	( )
Dawa inayouzwa bila masharti	( )
Dawa ya tiba yenye madhara ya kulevya	( )
Jina la dawa	…………………………………………………………………
Kiambata hai/viambata hai cha dawa na nguvu yake	……………………………………………………………... ………………………………………………………………… ……………………………………………………………….. ……………………………………………………………….
Namba ya usajili	
Aina ya nyenzo ya tangazo	(weka alama ya vema pale inapofaa)
Bango ( ) Kipeperushi ( ) Sinema/Bango la nje ( )	
Bango la Ndani/Kwenye Usafiri wa umma ( ) Magazeti ( )	
Machapisho ( ) Tangazo la sauti ( )	
Tangazo la video ( ) Nyinginezo( ), Tafadhali fafanua	
Kundi linalotangaziwa (umma au wataalam wa afya): Tafadhali fafanua …………………………………	
Njia ya kusambaza tangazo husika: ………………………………………	

Aina ya ombi	Ombi jipya ( )
	Ombi la kuhuisha ( )
Iwapo ni ombi la kuhuisha tafadhali ainisha kama kuna mabadiliko yoyote yaliyofanyika	…………………………………………………
	………………………………………………….

Fomu hii iambatishwe na:

ZINGATIA: Tafadhali weka alama ya√ au X kwenye orodha ya uhakiki

Nakala ya tangazo linalopendekezwa (Maandishi, Mchoro, Kanda ya sauti, CD, VCD, Kaseti ya Video.)	( )
Matumizi ya dawa kama ilivyoainishwa kwenye muhtasari wa sifa za dawa (inapohitajika)	( )
Nakala ya taarifa au tafiti zilizotajwa kwenye tangazo. (Zingatia: Mamlaka inaweza kuomba taarifa za ziada zikihitajika)	( )
Nakala ya idhini iliyopita (*kwa ombi la kuhuisha*)	( )

Tamko la mwombaji

Mimi, …………………………………………… ninathibitisha kuwa maelezo niliyotoa kwenye ombi hili ni ya kweli na sahihi. **Saini:** …………………………...………… Tarehe……………………………..................

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 7 (4))

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

KIBALI CHA MATANGAZO

Nambari ya kibali: ……………………

Kibali kimetolewa kwa ajili ya matangazo ya dawa kama ilivyoainishwa hapa chini; -

Jina la mwenye kibali……………….
Anuani………………………………...
…………………………………………

Jina la kibiashara la dawa	Jina la jenesi	Nyenzo za matangazo	Namba ya usajili	Hadhara inayolengwa

Kibali hiki kimetolewa leo………………………... na kitaendelea kuwa hai hadi ….………………………

Jina na Saini
MKURUGENZI MKUU

Masharti ya kibali:

1. Dawa itaendelea kutimiza matakwa ya usajili kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219.
2. Kibali hiki kirudishwe kwa Mamlaka inapotokea kimefutwa, kimebatilishwa au usajili wa dawa husika umeondolewa au kukoma au Mkurugenzi Mkuu anapoona inafaa kufanya hivyo.
3. Nyenzo ya matangazo inatimiza masharti kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219 na Kanuni zake.

4. Mwombaji atahakikisha ombi la kuhuisha linawasilishwa ndani ya siku thelathini kabla ya kibali kukoma.
5. Mabadiliko yote kwenye tangazo lililoidhinishwa yatatolewa taarifa kwa Mamlaka na kutekelezwa baada ya kuidhinishwa na Mamlaka.
6. Mamlaka ina haki ya kufuta au kubatilisha kibali hiki pale ambapo mwombaji atakiuka masharti ya sheria na kanuni zilizowekwa, au kwa maslahi ya umma.

JEDWALI LA TATU

(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 27 (1) na 28 (2))

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA MAONESHO YA BIASHARA, MAKONGAMANO NA MIKUTANO MINGINE

ZINGATIA: Ni kosa kutoa taarifa ya kupotosha au tamko la uongo.

(Taarifa zote zinazotolewa katika fomu hii na mwombaji zinapaswa zichapwe au ziandikwe kwa herufi kubwa)

Taarifa za mwombaji

Jina la mwombaji:	
Anuani:	
Postikodi:	
Nambari ya simu ya mezani:	
Nambari ya simu ya mkononi:	
Barua pepe:	
Akaunti ya mtandao wa kijamii (*kama inahusika*)	

Taarifa za mdhamini (kama ni tofauti na za mwombaji)

Jina la mdhamini:	
Anuani:	
Postikodi:	
Nambari ya simu ya mezani:	
Nambari ya simu ya mkononi:	
Barua pepe:	

Taarifa za tukio

Aina ya tukio	Weka alama ya vema panapohusika	Sehemu ya tukio	Hadhara inayolengwa	Tarehe ya tukio
Maonesho ya kibiashara				
Maonesho mengine				
Kongamano				
Mikutano mingine (*Tafadhali ainisha*)				

Taarifa za dawa

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (Kanuni za Udhibiti wa Matangazo ya Dawa za Binadamu na Mifugo)

Na.	Jina la dawa	Hali ya usajili		Namba ya usajili	Aina ya nyenzo ya matangazo
		Imesajiliwa	Haijasajiliwa *(ainisha idadi ya sampuli)*		

Zingatia: Aina ya nyenzo za matangazo inahusisha: Bango, Kipeperushi, Bango la nje, Machapisho, sampuli za dawa n.k.

Tukio hili litafanyika ……………………… (taja sehemu) kwa kipindi cha (muda) …………………..

Fomu hii iambatishwe na:
Tafadhali weka alama ya vema au X kwenye orodha ya uhakiki

( ) Nakala ya tangazo litakalotumika kwenye maonesho
( ) Nakala ya andiko la mada itakayowasilishwa kwenye mkutano au kongamano

Tamko la mwombaji

Mimi, ………………………………………………………………………. ninathibitisha kuwa maelezo niliyotoa kwenye ombi hili ni ya kweli na sahihi.

Saini: ……………………………………   Tarehe: …………………………………

JEDWALI LA NNE

(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 27 (2) na 28 (1))

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

KIBALI CHA MAONESHO, MAKONGAMANO NA MIKUTANO MINGINE

Namba ya kibali: ……………………

Kibali kinatolewa kwa ajili ya matangazo ya dawa kwenye maonesho ya kibiashara, makongamano au mikutano mingine kama ilivyoainishwa hapa chini; -

Jina la mwenye kibali ……………..………….
Anuani………………………………………...
…………………………………….........….

Aina ya tukio	Sehemu ya tukio	Hadhara inayolengwa	Tarehe ya tukio
Maonesho ya kibiashara			
Maonesho mengine			
Kongamano			

Kibali hiki kimetolewa leo……………………….. na kitaendelea kuwa hai hadi ….………………………

Jina na Saini
MKURUGENZI MKUU

Masharti ya kibali:

1. Bidhaa zitakazotangazwa zinakidhi matakwa yaliyoainishwa kwenye Sheria ya Dawa Vifaa Tiba, Sura 219.
2. Kibali hiki kirudishwe kwa Mamlaka inapotokea kimefutwa, kimebatilishwa au usajili wa dawa husika umeondolewa au kukoma au Mkurugenzi Mkuu anapoona inafaa kufanya hivyo.
3. Nyenzo ya matangazo inatimiza masharti kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219 na Kanuni zake.
4. Mamlaka ina haki ya kufuta au kubatilisha kibali hiki iwapo mwombaji atakiuka masharti ya sheria na kanuni zilizowekwa, au kwa maslahi ya umma.

JEDWALI LA TANO

(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 16 (2) na 20 (2))

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

NOTISI YA KUSITISHA AU KUFUTA KIBALI CHA MATANGAZO

Kwa mujibu wa kanuni ya 16 (2) na 20 (2) ya Kanuni za Udhibiti wa Matangazo ya Dawa za Binadamu na Mifugo, notisi ya kusitisha au kufuta kibali namba ………………… cha matangazo ya dawa inatolewa kwa…………………………………kwa sababu zilizoainishwa hapa chini; -

1.……

2.……

3.……

Kusitishwa kwa kibali hiki kutakuwa kwa kipindi cha siku ……………….. kutoka tarehe ya notisi hii na kunaweza kuondolewa iwapo marekebisho stahiki yamefanyika kama ilivyoelekezwa na Mamlaka

Imetolewa siku ya tarehe……………..ya mwezi ……………………mwaka ………………………..

Jina na Saini
Mkurugenzi Mkuu

JEDWALI LA SITA

(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 37 (3))

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

FOMU YA KUFIFILISHA MAKOSA

TMDA Namba...............
Kituo ....
Tarehe ....

Mimi, ... (jina) wa .... (anuani) ninakiri kuwa nimekiuka kanuni .... (taja masharti ya kanuni iliyokiukwa) kwa .... (weka maelezo ya makosa yaliyofanyika) na ninakiri kwamba, badala ya kushtakiwa kwa kufanya makosa hayo, kwa ridhaa yangu mwenyewe, ninakubali kuwa, makosa hayo yafifilishwe chini ya kanuni ya 37 ya Kanuni za Udhibiti wa Dawa za Binadamu na Mifugo za mwaka ………….. na …………………………………………………….. (taja jina la Afisa anaefifilisha makosa)

NA mimi, ... (jina na cheo cha Afisa anaefifilisha makosa), kwa kutumia mamlaka niliyopewa chini ya kanuni ya 37 ya Kanuni za Udhibiti wa Dawa za Binadamu na Mifugo za mwaka…………, naagiza kwamba

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (Kanuni za Udhibiti wa Matangazo ya Dawa za Binadamu na Mifugo)

.... (jina la mkosaji) alipe jumla ya shilingi za kitanzania ....kwa namna ya kufifilisha makosa, na mali/vidhibiti vifuatavayo vimetaifishwa na Serikali.

(Orodha ya bidhaa na nyenzo za matangazo zilizotaifishwa)

....
.

....
.

……………………………………………………………………………………………………..

Leo tarehe .... ya mwezi ...., mwaka ....

....

(Saini ya Mkosaji)   **(Saini ya Afisa)**

....
....

(Shahidi)   **(Shahidi)**

Tarehe…………………………. Jina wa Jengo…….……………………….……………….…………………..…………,

wa anuani na namba za simu ..……………….……………………………………….., ……………………………………..

mimi,……………………………………..………….. (jina la mmiliki au msimamizi) nakubali kuwa nimevunja sheria kifungu ....cha Sheria yaDdawa na Vifaa Tiba, Sura 219

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (Kanuni za Udhibiti wa Matangazo ya Dawa za Binadamu na Mifugo)

kwa………………………………………………………………………………………………………
……..……………………..

(eleza kosa) na nakubali kuwa badala ya kuhukumiwa kwa kosa hili kwa ridhaa yangu mwenyewe nakubali kulipishwa chini ya kanuni ya 12 ya Ada na Tozo ya TMDA ya mwaka 2021

Mimi..., ... (taja jina na wadhifa/cheo chako) wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa, katika kutekeleza majukumu niliyopewa kwa mujibu wa kanuni ya Ada na Tozo, TN 686, natoa maelekezo kuwa …………………………………....(jina la mtuhumiwakulipa kiasi cha shilingi .... ambapo (TZS……………………) kwa njia ya kufifilisha na TZS.…..……………..na asilimia 25 ya thamani ya bidhaa zilizokamatwa zilipwe kama fedha za kuteketeza mzigo, na silimia 2% kama FOB na asilimia 15% kama adhabu ya tozo ambayo haikulipwa kwa bidhaa ambayo imeingizwa nchini bidhaa ambazo ambazo zimeorodheshwa kwenye fomu zinataifishwa na serikali.

Leo tarehe……………..…siku ya …………………………………………………….. 20........................

…………………………………
……………………………………………

(Saini ya mkosaji) (Saini ya mtumishi wa TMDA aliyehusika)

…………………………………. ……………………………….

(saini ya shahidi) (Saini ya shahidi

ZINGATIA:

Fomu hii itatolewa nakala na fomu halisi atapatiwa m

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (Kanuni za Udhibiti wa Dawa za Binadamu na Mifugo)

Dodoma, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
Waziri wa Afya